



**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA MAKAMU WA RAIS**



**BARAZA LA TAIFA LA HIFADHI NA USIMAMIZI WA
MAZINGIRA**

**MKUTANO WA WADAU JUU YA UDHIBITI WA KELELE NA MITETEMO
UTAKAOFANYIKA KATIKA UKUMBI WA MIKUTANO WA KIMATAIFA WA
JULIUS NYERERE (JNICC) TAREHE 14 APRILI, 2023 SAA 3:00 ASUBUHI.**

Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC) kwa kushirikiana na Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam wameandaa Mkutano juu ya udhibiti wa Kelele na Mitetemo kwa wamiliki wa kumbi za starehe, bendi, baa na wadau wengine wa muziki utakaofanyika katika Ukumbi wa Mikutano wa Kimataifa wa Julius Nyerere (JNICC) tarehe 14 aprili, 2023.

Lengo la Mkutano huo ni kukuza uelewa juu ya matakwa ya Kanuni za Usimamizi wa Mazingira (Viwango vya Udhhibiti wa Kelele na Mitetemo) za mwaka 2015. Mgeni rasmi katika Mkutano huo ni Mhe. Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, CPA Amosi G. Makalla.

Hivyo, wadau wote mnaalikwa kushiriki Mkutano huu muhimu utakaotoa fursa ya kuainisha changamoto mbalimbali na kutoa maoni juu ya namna bora ya kuimarisha Uzingatiaji wa Kanuni na Viwango vya kelele na mitetemo.

*Imetolewa na Mkurugenzi Mkuu
Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira
12 Aprili, 2023*